Australian Government

# Uraia wa Australia

## Mapatano yetu ya Pamoja

Maelezo yote unayohitaji kujua ili kufanya majaribio ya uraia yako katika kitabu hiki: Hauhitaji kununua au kupata rasilimali zingine ya uraia kutoka mtu binafsi au mashirika ili kuweza kufaulu jaribio la uraia. Idara haikubaliani au kushauri rasilimali zozote ambazo zinaonekana kama zinaweza kukusaidia kufaulu jaribio la uraia.

© Jumuiya ya Madola ya Australia 2020

Mbali na koti la Jumuiya ya Madola, nyenzo zote zilizowasilishwa katika chapisho hili hutolewa chini ya haki ya Creative Commons wa 4.0 wa leseni ya kimataifa katika https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/legalcode.

Hii ina maana kuwa ruhusa hii inatumika tu kama ilivyoandikwa kwenye nyaraka hii.

Maelezo ya masharti husika ya leseni yanapatikana kwenye tovuti ya Creative Commons katika https://creativecommons.org/ kama ni kanuni kamili ya kisheria kwa leseni ya CC BY 4.0 katika https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/legalcode.

**Matumizi ya Silaha ya Koti**

Sheria ambazo Koti la Silaha hutumika ambazo zimeelezwa kwenye tovuti ya Idara ya Waziri Mkuu na Kabineti—https://www.pmc.gov.au/government/commonwealth-coat-arms.

**Wasiliana nasi**

Kutuuliza kuhusu leseni na matumizi ya nyaraka unaweza kufanya kwa:

Tawi la Habari na Ushirikiano
Idara ya Mambo ya Ndani
PO Box 25
BELCONNEN ACT 2616

**Kanusho**

Watu wa Aborigino na Torres Strait Islander watakaosoma wanaonywa kwamba chapisho hili lina picha na/au vitu vinavyohusiana na watu waliokufa.

# Yaliyomo

Ujumbe wako 2

## Sehemu ya majaribio

Sehemu ya 1 Australia na watu wake 7

Sehemu ya 2 Imani za demokrasia, haki na uhuru wa Australia 17

Sehemu ya 3 Serikali na Sheria katika Australia 23

Sehemu ya 4 Maadili ya Australia 33

Faharasa ya sehemu inayoweza kujaribiwa 40

## Sehemu isiyoweza kujaribiwa

Sehemu ya 5 Australia leo 48

Sehemu ya 6 Historia yetu ya Australia 63

Faharasa ya sehemu isiyoweza kujaribiwa 84

Kwa maelezo zaidi 86

Shukrani 88

# Ujumbe kwako

Hongera kwa kuchagua kuwa raia wa Australia. Inahitaji ujasiri, kuvumilia na kujitolea kuishi katika nchi geni na kuhusika kikamilifu kama raia. Tunathamini mchango wako kwa jamii yetu yenye amani na demokrasia.

Uraia wa Australia ni hatua muhimu katika hadithi yako ya uhamiaji. Kuwa raia wa Australia inamaanisha kwamba unaendelea kujitolea kwa Australia na yote ambayo nchi hii inamaanisha. Pia ni mwanzo wa uanachama wako rasmi wa jamii ya Australia. Ni hatua ambayo itakuwezesha kusema 'Mimi ni Mwaustralia'.

Uraia wa Australia ni fursa inayotoa thawabu anuwai. Kwa kuwa raia wa Australia, unaungana na jamii ya kipekee ya kitaifa. Nchi yetu imejengwa kwenye michango michanganyiko ya watu wetu wa Aboriginal and Torres Strait, taasisi za kidemokrasia tulizozirithi kutoka Uingereza, na wahamiaji hapa kutoka ulimwengu wote. Tunasherehekea utofauti wetu na kwa wakati huo huo, tunang'angan'ia taifa lenye umoja na usawa.

Nguvu ya jamii ya Australia inamaanisha kwamba tunafanya kazi pamoja kutatua matatizo na kufanya Australia nchi nzuri ilivyo. Tuna mfumo thabiti wa serikali na Waaustralia wanaheshimu mamlaka na sheria za serikali. Uthabiti wetu, utamaduni wetu na sheria zetu zimeundwa na historia yetu. Kwa kujiunga na jamii ya Australia, utarithi historia hii na utakuwa kwenye nafasi ya kuichangia.

Australia ni nchi ya zamani. Ni kubwa na ya kipekee. Ni nchi ya misitu ya mvua na misitu; ya ufuo na majagwa; na miji na mashamba. Tamaduni zetu za asili ndizo za zamani kabisa zinazoendelea katika ulimwengu. Sisi pia ni taifa changa; taifa la wahamiaji. Makazi ya waulaya hapa Australia yalianza mnamo 1788 na tunaendelea kukaribisha wahamiaji wapya leo.

Watu kutoka kwa zaidi ya nchi 200 wamefanya Australia kuwa nyumbani kwao. Hivyo basi, jamii yetu ni moja ya zile zilizo anuwai zaidi ulimwenguni. Australia inajumuisha asili ya kikabila na kitamaduni anuwai na umoja wa kitaifa. Uraia ni umoja unaotuunganisha sisi sote.

Australia ni demokrasia. Uraia hukupa fursa ya kuhusika kikamilifu katika kujenga taifa letu la kidemokrasia. Inamaanisha kwamba uko tayari kutimiza wajibu wako kama mwanachama rasmi wa jamii ya Australia. Watu wa Australia wanaamini uadilifu na uhuru wa kila mtu, nafasi sawa kwa wanaume na wanawake na utawala wa sheria. Uraia wa Australia ni juu ya kuishi kutoka kwa thamani hizi katika maisha yako ya kilasiku.

# Kuwa raia wa Australia

Kuwa raia wa Australia ni mchakato muhimu ambapo mtu huahidi uaminifu wao kwa Australia na watu wake, halafu ndipo anastahili kutumia haki na majukumu yao kama raia wa taifa letu.

## Jaribio la uraia wa Australia

Jaribio la uraia wa Australia limeundwa kuchunguza ikiwa una ufahamu wa kutosha juu ya Australia na mfumo wake wa kidemokrasia, imani na maadili, na majukumu na haki za uraia.

Jaribio la uraia ni jaribio la kompyuta lenye majibu mengi kwa Kiingereza. Unajumuisha maswali 20 yaliyochaguliwa kwa nasibu; na kufikia tarehe 15 Novemba 2020, itajumuisha pia maswali matano yanayohusu maadili ya Australia.

Ili kupita mtihani, lazima ujibu maswali yote matano ya maadili kwa usahihi, na alama ya angalau asilimia 75 kwa jumla.

Majaribio ya uraia hufanywa katika ofisi za Idara ya Uhamiaji na Uraia kote Australia. Majaribio pia yamepangwa katika maeneo kadhaa kote katika mikoa wa Australia na katika baadhi ya balozi za nchi za ng'ambo.

## Kujiandaa kwa jaribio la uraia wa Australia

Kujiandaa kwa jaribio la uraia utahitaji kusoma kitabu hiki cha msaada, *Araia wa Australia: Mapatano yetu ya Pamoja*

Kitabu hiki cha msaada kina sehemu inayoweza kujaribiwa na isiyoweza kujaribiwa.

### Sehemu inayoweza kujaribiwa

Maelezo yote unayohitaji kujua kupita majaribio ya uraia yako katika sehemu nne za kwanza za kitabu hiki:

- Semehu ya 1 – Australia na watu wake
- Sehemu ya 2 – Imani ya demokrasia, haki na uhuru wa Australia
- Sehemu ya 3 – Serikali na sheria katika Australia
- Sehemu ya 4 – Maadili ya Australia

Utahitajika kujua na kuelewa maelezo katika sehemu inayoweza kujaribiwa ili kujibu maswali katika jaribio la uraia.

### Sehemu isiyoweza kujaribiwa

Sehemu isiyoweza kujaribiwa ina maelezo muhimu ambayo yatakusaidia kuelewa historia na utamaduni wa Australia. Hautajaribiwa juu ya maelezo haya.

- Sehemu ya 5 – Australia leo
- Sehemu ya 6 – Historia yetu ya Australia

### Maswali ya mazoezi

Mwisho wa sehemu inayoweza kujaribiwa, kuna maswali 20 ya mazoezi ili kukusaidia kujiandaa kwa jaribio la uraia.

### Faharasa

Kuna faharasa (orodha ya maneno kuu na maana yao) mwisho wa sehemu zinazoweza kujaribiwa na zisizoweza kujaribiwa.

### Kwa maelezo zaidi

Nyuma ya kitabu cha rasilimali, unaweza kupata ushauri juu ya wapi pa kupata habari zaidi.

### Msaada wakati wa jaribio la uraia wa Australia

Inatarajiwa kwamba raia wengi wanaotarajiwa wa Australia watakuwa na ustadi wa kusoma na kuandika unaofaa kukamilisha jaribio la uraia bila msaada. Teknolojia ya maandishi-kwa-hotuba, ambayo unaweza kutumia kusikiliza maswali na uchaguzi wa majibu, inapatikana pia.

### Jaribio la uraia wa Australia

Ikiwa utafanya jaribio, tutaendelea kushughulikia maombi yako. Ikiwa maombi yako yamepitishwa na unahitajika kuhudhuria sherehe ya uraia, utapokea barua ya mwaliko kuhudhuria sherehe hiyo.
Kwa ujumla, sherehe yako itafanyika ndani ya miezi sita tangu wakati maombi yako yameidhinishwa.

# Kiapo cha Uraia wa Australia

Ni muhimu kwa raia wote wa Australia kuelewa haki zetu na wajibu wetu na inamaanisha nini kuwa raia, ikiwa sisi ni wa Australia kwa kuzaliwa au kwa kuchagua. Hii ni muhimu kwa mafanikio endelevu ya taifa letu.

Wakati unahudhuria hafla ya uraia wa Australia, utachukua Kiapo cha Uraia wa Australia.

Kwa kufanya hivyo, unajitolea kwa umma kwa Australia na kukubali wajibu na fursa za uraia.

Hiki ndicho kiapo utakachochukua:

***Kuanzia wakati huu na kuendelea, chini ya Mwenyezi Mungu,****

***Ninaapa uaminifu wangu kwa Australia na watu wake,***

***ambao ninashiriki imani yao ya demokrasia,***

***ambao ninaheshimu haki zao na uhuru wao, na***

***ambao nitafuata na kutii sheria zao.***

* Mtu anaweza kuchagua kiwa atatumia maneno ‘chini ya Mwenyezi Mungu’.

Unaposoma kitabu hiki, utapata kuelewa kikamilifu maana ya Kiapo na jinsi unaweza kuboresha wajibu wako katika jamii ya Australia.



# Hafla ya uraia wa Australia

Hafla za Uraia wa Australia zinaweza kuwa ndogo, zikihusisha tu watu wachache, au zinaweza kuwa kubwa sana, zikihusisha mamia au hata maelfu ya watu. Undani wa kuhisi na kujivunia kati ya raia wageni na maafisa huifanya iwe karamu yenye raha sana.

Katika mwanzo wa hafla ya uraia, unaweza kukaribishwa na mwakilishi wa watu wa Aboriginal and Torres Strait Islander ambao ni wamiliki wa kitamaduni wa ardhi katika eneo lako. Itifaki hii ya Karibu kwa Nchi imekuwa ikifanywa na Waaustralia wa Asili kwenye makazi yao ya jadi kwa maelfu ya miaka. Utasikia maneno ya kukaribisha na kuhimiza kutoka kwa viongozi wengine wa jamii ya eneo lako au wawakilishi wa serikali.

Utasoma au kurudia Kiapo cha Uraia wa Australia kwa sauti na watu wengine ambao wamechagua kuwa raia wa Australia. Hivi ni sehemu muhimu sana ya hafla. Hutakuwa raia wa Australia mpaka umeapa kiapo chako cha kuijitolea kwa Australia.

Unakaribishwa kuleta kitabu au somo takatifu ili kushika wakati unapoapa, lakini sio lazima ufanye hivyo.

Viongozi kutoka kwa jamii yako au wawakilishi wa serikali watatoa hotuba fupi juu ya maana ya uraia. Utapokea Cheti cha Uraia wa Australia na unaweza pia kupokea zawadi ndogo kutoka kwa jamii. Kila mtu ataimba wimbo wa taifa wa Australia 'Endeleza Australia bila mapendeleo (Advance Australia Fair)'.

Baada ya hafla ya uraia, utakuwa na fursa ya kukutana na kusherehekea na wenzako wa Australia.

Tunakutakia kila la heri katika kuwa raia wa Australia na katika kutafuta maisha yenye amani na yenye mazao hapa Australia.

## Kwa maelezo zaidi

Tembelea tovuti ya uraia wa Australia kwenye www.citizenship.gov.au.





# Sisi husherehekea mwanzo wa mwaka mpya



# SEHEMU YA KWANZA

## Australia na watu wake

# Australia na watu wake

Katika hafla ya uraia, unaapa uaminifu wako kwa Australia na watu wake. Kwa hivyo ni muhimu kwako kuwa na kuelewa kwa jamii na idadi ya watu wa Australia, pamoja na urithi wetu wa asili. Ni muhimu pia kwako kuelewa historia ya Australia na jinsi ambavyo tumekuza kuwa taifa thabiti na lenye mafanikio ya kitamaduni.

Katika sehemu hii, utasoma juu ya baadhi ya matukio ambayo yamechangia hadithi yetu. Kuna maelezo kuhusu majimbo yetu na wilaya yetu, na kuna maelezo kuhusu tamaduni na ishara ambazo tunatambua kwa kujivunia kama kuwa ya Australia kipekee.

## Watu wa Aboriginal na Torres Strait Islander

Wakaazi wa kwanza wa Australia ni watu wa Aboriginal and Torres Strait Islander, ambao wana tamaduni na mila zinazoendelea zaidi ulimwenguni.

Kihistoria, watu wa asili wanatoka katika nchi kuu ya Australia na Tasmania. Rekodi ya akiolojia inaonyesha ambao watu wa Aboriginal waliofika Australia kati ya miaka 65,000 na 40,000 iliyopita; Walakini, watu Aboriginal wanaamini wao ni msingi wa hadithi za uumbaji wa ardhi hii, na hadithi zao za uumbaji zinaanza na mwanzo wa wakati. Watu wa visiwa vya Torres Strait wanatoka kwenye visiwa kati ya ncha ya Queensland na Papua New Gunea.

Watu wa Aboriginal and Torres Strait Islander wana imani na tamaduni sawa ambazo bado huwaongoza leo. Wana uhusiano wa ndani na ardhi ambayo huoneshwa katika hadithi, sanaa na kucheza kwao. Tamaduni za asilia ni tofauti na ni sehemu muhimu ya kitambulisho cha kitaifa cha Australia.

Kwa habari zaidi kuhusu kuhusu watu wa Aboriginal na Torres Strait Islander inaweza kupatikana *Sehemu ya 5, Australia leo* na *Sehemu ya 6, Historia yetu ya  Australia*.

## Siku za mapema za makazi ya Waulaya

Makazi ya Ulaya yaliaanza wakati meli za kwanza za wafungwa, ambazo zilikuja kujulikana kama "Kundi la kwanza la Meli (First Fleet), kuwasili kutoka Briteni mnamo 26 Januari 1788.

Wakati huu sheria za Briteni zilikuwa kali na jela hazingeweza kuweka idadi kubwa ya watu waliofungwa kwa uhalifu wao. Kuweza tatizo hili, Serikali ya Briteni iliamua kusafirisha wafungwa hadi upande mwingine wa ulimwengu; kwa koloni mpya ya New South Wales.

Gavana wa kwanza ya koloni ya New South Wales alikuwa Captain Arthur Phillip. Koloni ilistahimili na vile wafungwa zaidi na wakazi huru walipofika, ilikuwa kubwa na kuendelea. Koloni zaidi zilianzishwa katika sehemu zingine za Australia.

Wakazi huru wa mapema kutoka Briteni Kuu na Ireland. Urithi wa Briteni na Irishi umekuwa na ushawishi mkubwa kwa historia ya Australia, tamaduni na siasa.

Mnamo 1851, dhahabu iligunduliwa katika koloni za New South Wales na Victoria. Watu kutoka ulimwenguni kote walikuja kwa koloni hizi kujaribu bahati yao kwa kutengeneza mali. Watu wa Uchina waliofika wakati huo walikuwa kundi la kwanza la wahamiaji ambao hawakutoka Ulaya. Katika miaka 10, idadi ya watu wa Australia ilikuwa zaidi ya mara mbili.



# Taifa la Australia

Mnamo 1901, koloni ziliungana kuwa shirikisho la majimbo liitwalo Jumuiya ya Madola ya Australia. Ni mda huu ambapo taasisi zetu za kidemokrasia, ikiwa ni pamoja na bunge la taifa, serikali na Mahakama Kuu zilianzishwa chini ya Katiba mpya ya Australia. Mwaka 1901, idadi ya watu wa Australia ilihesabiwa kuwa karibu watu milioni nne. Nambari hii haikujumuisha watu wa Aboriginal na Torres Strait Islander, kwani haikuwa hadi baada ya Maazimio mnamo 1967 kwamba walijumuishwa katika makadirio rasmi ya idadi ya watu wa Australia.

Wakati wote wa nusu ya kwanza ya karne, viwango vya uhamaji vilipanda na kushuka. Kulikuwa na mipango ya kuhimiza wahamiaji wa Briteni ili kukaa hapa, na wengi walifanya hivyo.

Wimbi la uhamiaji usio wa Briteni ulikuja baada ya Vita vya II vya Dunia, wakati mamilioni ya watu huko Ulaya walilazimika kuacha nchi zao. Idadi kubwa ya watu wa Ulaya ilikuja Australia kujenga maisha mapya.

Katika miaka ya hivi karibuni, mipango yetu ya uhamaji na ukimbizi imeleta watu Australia kutoka ulimwenguni kote. Watu wamekuja hapa kuungana na familia, kuanza maisha mapya, au kutoroka umaskini, vita au kuadhibiwa.


Utofauti wa watu wa Australia umeongezeka katika karne mbili zilizopita. Jamii hii tofauti na yenye kufaulu inaongeza uhusiano wa Australia na ulimwengu. Wakati tunasherehekea anuwai ya watu wa Australia, tunalenga pia kujenga taifa la kushikana pamoja na yenye umoja.

Kiingereza ni lugha ya taifa la Australia. Ni sehemu ya utambulisho wa kitaifa. Kila mtu hapa Australia anahimizwa kujifunza na kutumia Kiingereza kuwasaidia kuhusika katika jamii ya Australia. Kuwasiliana kwa Kiingereza pia ni muhimu kwa kutafuta mapato na kufanya kazi Australia.

Lugha zingine pia zinathaminiwa, ikiwa ni pamoja na lugha zaidi ya 100 za Aboriginal na Strait Islander.

# Majimbo na wilaya za Australia


Jumuiya ya madola ya Australia ni shirikisho la majimbo na wilaya. Kuna majimbo sita na wilaya mbili za nchi kuu. Canberra ndio mji mkuu wa Australia, na kila jimbo na wilaya ya nchi kuu ina mji mkuu wake.




| Mkoa | Jimbo Mji mkuu |
|---|---|
| New South Wales (NSW) | Sydney |
| Victoria (Vic.) | Melbourne |
| Queensland (Qld) | Brisbane |
| Australia ya Magharibi (WA) | Perth |
| Australia ya Kusini (SA) | Adelaide |
| Tasmania (Tas.) | Hobart |
| **Wilaya** | **Jimbo Mji mkuu** |
| Australian Capital Territory (ACT) | Canberra |
| Northern Territory (NT) | Darwin |

## Majimbo

**New South Wales** ilikuwa koloni ya kwanza kuanzishwa na Briteni. Sydney ni mji mkuu wa New South Wales na ndio mji mkubwa zaidi wa taifa. Harbour Bridge na Opera House ya Sydney ni ikoni za kitaifa**.**



---

**Victoria** ndio jimbo ndogo zaidi la nchi kuu. Mji mkuu wa Victoria ni Melbourne. Majengo mengi mazuri huko Victoria yalijengwa kutoka kwa mali iliyoundwa na dhahabu ya 1850. Alama za Victoria ni pamoja na Uwanja wa Kriketi wa Melbourne, Mitume 12, Jengo la Maonyesho la Kifalme .



---

**Queensland** ni mkoa wa pili kwa ukubwa. Mji mkuu wa Queensland ni Brisbane. Torres Strait Islands wako kaskazini mwa mkoa na Great Barrier Reef maarufu ulimwenguni inapita kando mwa pwani yake ya mashariki. Queensland ina misitu ya mvua ya kitropiki, maeneo yenye joto ya pwani na nchi kavu mara nyingi



---

**Australia Magharibi (Western Australia)** ndilo mkoa mkubwa zaidi. Perth ni mji mkuu wa Australia ya Magharibi. Mashariki mwa jimbo ni jangwa sana, wakati kusini-magharibi ni eneo lenye ukulima na kukuza mvinyo. Jimbo hilo ni nyumbani kwa miradi mingi kubwa. Alama za Australia Magharibi ni pamoja na Pwani ya Ningaloo, Mto wa Margaret, na sehemu ya Kimberley.



---

**Australia Kusini** ina pwani isiyo ya tambarare na wilaya nyingi za mvinyo zinazojulikana. Adelide, mji mkuu, una mifano mingi ya usanifu majengo wa kikoloni. Alama za Australia Kusini ni pamoja na Bonde la Barossa na Njia za Flinders



---


**Tasmania** ndilo mkoa mdogo zaidi, imetengwa kutoka kwa nchi kuu na Bass Strait. Mji mkuu wa Tasmania ni Hobart. Kisiwa kina mandhari ya jangwa ambayo hayajaharibiwa. Alama za Tasmanian ni pamoja na Mountain Cradle, Port Arthur, na Bay of Fires



---

## Wilaya

**Wilaya Kuu ya Australia (Australian Capital Territory)** iko katikati ya Sydney na Melbourne. Ni eneo la mji mkuu wa taifa, Canberra. Canberra ni nyumbani kwa taasisi muhimu za kitaifa, kama vile Jumba la Bunge na Mahakama Kuu ya Australia.



---

**Wilaya ya Kaskazini** ina tropiki katika kaskazini na mchanga mwekundu wa jangwa huko kusini. Darwin ndio mji mkuu. Alama za Wilaya ya Kaskazini ni pamoja na Uluru, Kata Tjuta na Kings Canyon.





# Mila

## Utaratibu wa Ukaribisho kwenye nchi na Kushukuru kama utaratibu

Ukaribisho wa kwenye Nchi ni utamaduni unachofanywa na msimamizi wa Aboriginal or Torres Strait Islander wa mkoa huo, wakati wa kukaribisha wageni kwenye ardhi yao ya jadi. Hii hufanywa kama jadi ili kuhakikisha kuwa wageni wana safari salama na ulinzi wakati wakiwa kwenye ardhi hiyo.

Ukaribisho wa kwenye Nchi unaweza kuchukua njia nyingi, pamoja na nyimbo, densi, sherehe za kuvuta au hotuba kwa lugha ya jadi au Kiingereza.

Ukaribisho wa kwenye Nchi ni jambo la kwanza la katika kufungua tukio.

Kushukuru kwa ajiri ya Nchi ni nafasi kugundua kuwa mkutano huo uko kwenye ardhi ya Kisiwa cha Aboriginal au Torres Strait; waheshimu Walezi wa Jadi, haswa Wazee wa zamani na wa sasa; na kuwaheshimu watu wa Aboriginal na wa Torres Strait Islander waliokuwepo.

Kushukuru Nchi kwa kawaida hutolewa kama sehemu ya Ukaribishaji na Utunzaji wa mahali katika mikutano na hafla. Mtu yeyote anaweza kutoa Kushukuru kwa Nchi. Katika mikutano/hafla, hii kwa ujumla inaweza kufanywa na Mwenyekiti au Mkubwa wa Sherehe.

Matendo haya hufanywa kuonyesha heshima kwa watu wa Aboriginal and Torres Strait Islander.



# Siku muhimu kwa Australia

## Siku ya Australia

Mnamo 26 Januari kila mwaka, sisi husherehekea Siku ya Australia. Siku ya Australia ni sikukuu ya umma katika kila jimbo na wilaya hapa Australia. Ni kumbukumbu ya kuwasili kwa Meli ya Kwanza kutoka Great Britain mnamo mwaka 1788.

Kwenye Siku ya Australia, jamii za Australia kote zinafikiria historia yetu, na watu ambao wamechangia mafanikio yetu ya pamoja. Ndio tukio kubwa zaidi la kila mwaka hapa Australia.

Siku ya Australia ni juu ya kukiri na kusherehekea mchango ambao kila Mwaustralia hufanya kwa taifa letu la kisasa na lenye nguvu: kutoka watu wa Aboriginal na Torres Strait Islander-ambao wamekuwa hapa kwa takriban miaka 65,000 - kwa wale ambao wameishi hapa kwa vizazi, na wale ambao wametoka pande zote za ulimwengu kuiita nchi yetu nyumbani. Siku ya Australia husherekewa kwa matukio kuzunguka Australia, ikiwa ni pamoja sherehe maalum za uraia.

Usiku wa kuamkia Siku ya Australia, Waziri Mkuu hutangaza Tuzo ya Mwaustralia wa Mwaka huo huko Canberra.

## Siku ya Anzac

Siku ya Anzac hukumbukwa mnamo 25 Aprili kila mwaka. Siku ya Anzac imepewa jina baada ya Askari wa New Zealand na Australia, ambao walitua huko Gallipoli huko Uturuki wakati wa Vita vya Dunia vya 1 mnamo 25 Aprili 1915.

Siku ya Anzac ni siku ya zito wakati sisi hukumbuka thabihu ya Waaustralia wote ambao walitumikia na kufa siku za vita, shughuli za mizozo na utafutaji amani. Tunaheshimu pia ujasiri na kujitolea kwa wanajeshi wote na wanawake na kutafakari juu ya maana nyingi za vita tofauti.

Habari kuhusu siku zingine muhimu za kitaifa na sherehe zinaweza kupatikana ndani *Sehemu ya 5, Australia leo.*

# Bendera za Australia

Bendera ya Kitaifa ya Australia ni bendera rasmi ya taifa letu. Australia ina bendera tatu rasmi.: Bendera ya Kitaifa ya Australia, Bendera ya Watu wa Asili ya Australia na Bendera ya Watu wa Visiwa vya Torres Strait.

Kila mkoa na eneo pia zina bendera yake zenyewe, ambazo zinaweza kutazamwa kwenye ukurasa wa 11.

## Bendera ya Taifa la Australia

Bendera ya Taifa ya Australia ni bluu, nyeupe na nyekundu.

- 'Union Jack' , ambayo ni bendera ya Uingereza, iko katika sehemu ya kona juu kushoto. Inawakilisha historia yetu ya makazi ya Waingereza na sheria na taasisi tulizozimiliki kama matokeo.
- Nyota ya Jumuiya ya madola iko chini ya Union Jack. Nyota ina ncha saba, kila ncha inawakilisha mojawapo ya mikoa sita na moja ya wilaya.
- Msalaba wa Kusini (Southern Cross), sehemu ya kulia, ni kundi la nyota tunazoona angani upande wa kusini.



## Bendera ya Watu wa asili ya Australia

Bendera ya Watu wa asili ya Australia ni nyeusi, nyekundu na manjano.

- Sehemu ya juu nusu ni nyeusi na inawakilisha watu wa Aboriginal wa Australia.
- Sehemu ya chini nusu ni nyekundu na inawakilisha ardhi, ambayo ina uhusiano wa kiroho.
- Mviringo wa manjano unawakilisha jua.



## Bendera ya Watu wa visiwa wa Torres Strait

Bendera ya Watu wa visiwa wa Torres Strait ni kijani kibichi, bluu, nyeusi na nyeupe.

- Mistari ya kijani kibichi inawakilisha nchi.
- Paneli ya bluu iliyo katikati inawakilisha bahari.
- Mistari nyeusi inawakilisha watu wa visiwa vya Torres Strait.
- Kitambaa cheupe cha kichwa cha Mchezaji kilicho katikati ni ishara ya watu wote wa visiwa vya Torres Strait.
- Ncha za nyota nyeupe zinatoa mfano wa vikundi vya kisiwa katika Torres Strait, na rangi nyeupe inawakilisha amani.



# Alama ya Australia

## Nembo ya Jumuiya ya Madola

Nembo ya Jumuiya ya Madola ndio ishara rasmi ya Jumuiya ya Madola ya Australia. Inaleta mfano wa umoja wa kitaifa. Inatambua mamlaka na mali ya Jumuiya ya Madola ya Australia.

- Ngao iliyoko katikati inawakilisha majimbo sita na shirikisho.
- Kangaroo na emu zinawakilisha ngao kila upande. Kangaroo ni wanyama asilia wa Australia.
- Nyota ya dhahabu ya Jumuiya ya Madola hukaa juu ya ngao.
- Mandhari nyuma ni ufito wa dhahabu, ua la kitaifa ya Australia.





## Maua ya kitaifa ya Australia

Maua ya kitaifa ya Australia ni ufito wa dhahabu. Mti huu mdogo hukua haswa katika kusini-mashariki Australia. Ina majani ya kijani kibichi na maua mengi ya manjano dhahabu wakati wa majira ya kuchipua. Kila jimbo na wilaya za Australia pia zina nembo yake ya maua.



## Rangi za kitaifa za Australia

Rangi za kitaifa za Australia ni kijani na dhahabu, rangi za ufito wa dhahabu. Sare za timu zetu za kitaifa za spoti kawaida ni kijani kibichi na dhahabu.



## Kito cha kitaifa cha Australia

Opali ndio kito cha kitaifa cha Australia. Katika hadithi ya Aboriginal, upinde wa mvua uligusa ardhi na kuunda rangi za opali.



# Wimbo wa taifa wa Australia

'Endeleza Australia bila Mapendeleo' (Advance Australia Fair) ndio wimbo wa taifa. Huwa inaimbwa kwenye hafla za umuhimu wa kitaifa, pamoja na kwenye sherehe za uraia wa Australia na hafla kuu za michezo.

## Advance Australia Fair

*Australians all let us rejoice,*
*For we are one and free;*
*We've golden soil and wealth for toil;*
*Our home is girt by sea;*
*Our land abounds in nature's gifts*
*Of beauty rich and rare;*
*In history's page, let every stage*
*Advance Australia Fair.*
*In joyful strains then let us sing,*
*Advance Australia Fair.*

*Beneath our radiant Southern Cross*
*We'll toil with hearts and hands;*
*To make this Commonwealth of ours*
*Renowned of all the lands;*
*For those who've come across the seas*
*We've boundless plains to share;*
*With courage let us all combine*
*To Advance Australia Fair.*
*In joyful strains then let us sing,*
*Advance Australia Fair.*



# SEHEMU YA PILI

## Imani za demokrasia, haki na uhuru wa Australia

# Imani za demokrasia, haki na uhuru wa Australia

Kwenye hafla ya uraia, unaapa kwamba utashiriki imani za demokrasia za Australia, na kwamba utaheshimu haki na uhuru wake. Ni muhimu kwamba uelewe imani hizi za demokrasia, na haki na uhuru ambao watu wote wa Australia wanazoheshimu.

Sehemu hii ya kijitabu hiki inaorodhesha imani hizi, haki na uhuru. Kwa maelezo zaidi tazama *Sehemu ya 4, maadili ya Australia*.

## Imani zetu za demokrasia

### Demokrasia ya bunge

Demokrasia ya bunge Mfumo wa serikali ya Australia ni demokrasia ya bungeni. Kama sehemu ya mwongozo, nguvu ya serikali inatoka kwa watu wa Australia kwa sababu raia wa Australia hupiga kura ya watu wa kuwawakilisha bungeni. Wawakilishi katika bunge lazima wajibu watu, kupitia Uchaguzi, kwa maamuzi wanayofanya.

### Utawala wa sheria

Waaustralia wote ni sawa chini ya sheria. Utawala wa sheria ina maana kwamba hakuna mtu, kundi au dini lililiko juu ya sheria. Kila mtu, ikiwa ni pamoja na watu wenye vyeo vya juu katika jamii ya Australia, ni lazima watii sheria za Australia. Hii ni pamoja na viongozi wa serikali, jamii na wa kidini, na watu wa biashara na polisi.

### Kuishi kwa amani

Tunajivunia kuishi katika nchi yenye amani na mfumo thabiti wa serikali. Tunaamini kwamba mabadiliko yanapaswa kutokea kupitia mjadala, ushawishi wenye amani na michakato ya demokrasia. Tunakataa uhasama kama njia ya kubadili mawazo ya mtu au sheria.

### Heshima kwa watu wote bila kujali asili

Muundo wa demokrasia wa Australia umeundwa kwa msingi wa kwamba kila mtu, bika kujali asili yao, ana haki na usawa chini ya sheria ya Australia. Waaustralia wote wanatarajiwa kutendea wenzao na uadilifu na heshima, bila kujali kabila lao, nchi asili, jinsia, mapendeleo ya kingono, hali ya ndoa, umri, ulemavu, urithi, tamaduni, siasa, mali na dini.



# Uhuru wetu

## Uhuru wa kuzungumza na uhuru wa kujielezea

Uhuru wa kusema ni msingi wa uadilifu wa Australia na hujengwa na muundo wa demokrasia ya Australia. Uhuru wa kuzungumza ina maana kwamba watu wanaweza kusema na kuandika wanachofikiria na kujadili mawazo yao na wengine. Kwa mfano, watu wanaweza kukosoa serikali, kupinga kwa amani maamuzi ya serikali na kufanya kampeni kubadili sheria, cha mhimu ni kuwa wakati wote bado wanatii sheria za Australia.

Uhuru wa kujielezea ina maana kwamba watu wanaweza kuonyesha maoni yao, ikiwa ni pamoja na kupitia sinema, muziki na fasihi. Watu wako huru kukutana katika mahali pa umma au pa siri kwa mjadala wa kijamii au kisiasa.

Wakati wote, hata wakati unashiriki katika uhuru wa kusema na uhuru wa kujieleza, sheria za Australia lazima zizingatiwe. Lazima tusheshimu uhuru wa watu wengine wa kuzungumza au kujielezea.

## Uhuru wa ushirika

Uhuru wa ushirika ni haki ya kuunda na kujiunga na vyama ili kutekeleza malengo ya kawaida. Kwa mfano, katika Australia watu wana uhuru wa kuungana na shirika la kisheria, kama vile chama cha kisiasa, chama cha wafanyikazi, kundi la kitamaduni au kijamii. Watu wanaweza pia kuamua kutojiunga nao na hawawezi kulazimishwa kufanya hivyo.

Waaustralia wanaweza kuja pamoja kupinga hatua ya serikali au shirika. Wakati wote, hata hivyo, sheria za Australia lazima kuzitii. Hii inamaanisha hayo maandamano lazima yawe ya amani, na lazima zisiumize mtu yeyote au kuharibu mali.

## Uhuru wa dini

Australia ina urithi wa Ukristo wa Judea, na Waaustralia wengi hujielezea kama Wakristo, lakini kuna watu nchini Australia kutoka dini zote kubwa.Australia ina sikukuu za umma kwa siku za Kikristo kama Ijumaa Kuu, Jumapili ya Pasaka na Siku ya Krismasi. Serikali na sheria vinawatendea raia kwa usawa, haijalishi dini au imani yao. Serikali hapa Australia ni ya kidunia, ikiwa na maana kwamba inaendeshwa mbali na makanisa au madini mengine. Australia haina dini rasmi ya kitaifa. Watu hapa Australia wako huru kufuata dini yoyote wanayochagua. Wanaweza kuchagua kutokufuata dini yoyote.

Wakati wote, hata wakati unahusika katika mazoea ya kidini, sheria za Australia lazima zizingatiwe. Pale panapokuwa na utata kati ya sheria ya Australia na ibada za madini, sheria ya Australia ndiyo inashinda.

# Usawa wetu

Kuna baadhi ya sheria hapa Austrakia ambazo hukakikisha mtu hatendewi tofauti na wengine kwa sababu ya jinsia yao, rangi, ulemavu au umri.

## Usawa wa kijinsia

Wanaume na wanawake wana haki sawa hapa Australia. Ni kinyume cha sheria kubagua mtu kwa sababu ya jinsia yake.

## Usawa wa fursa na 'sawa kwenda'

Waustralia wanathamini nafasi sawa katika jamii yetu; kile kinachoitwa 'usawa kwenda'. Hii inamaanisha kwamba kile mtu anafikia maishani mwake kinapaswa kuwa matokeo ya bidii yao na vipawa vyao, kazi na juhudi, kuliko mali na asili yao. Hii ni kuhakikisha kuwa hakuna tofauti rasmi za darasa katika jamii ya Australia.

# Wajibu na faida za Raia wa Australia

Unapokuwa raia wa Australia, utakuwa na wajibu na faida za ziada.

## Wajibu - ni nini utaipa Australia

Kama raia wa Australia lazima:

- kutii sheria za Australia.
- piga kura katika uchaguzi wa shirikisho na mkoa au wilaya, na katika kura ya maoni
- linda Australia ikiwa kutatokea hitaji
- tumikia baraza la wazee kortini ukiitwa kufanya hivyo

## Upendeleo - ni nini Australia itakupa

Kama raia wa Australia unaweza:

- piga kura katika uchaguzi wa shirikisho na mkoa au wilaya, na katika kura ya maoni
- kuomba watoto waliozaliwa ng'ambo kuwa raia wa Australia kwa ukoo
- kuomba kufanya kazi katika Huduma ya Umma au katika Jeshi la Ulinzi la Australia.
- kuwania uchaguzi wa bunge
- kuomba pasi ya Australia na kuingia tena Australia huru
- kupokea msaada kutoka kwa afisa wa Australia ukiwa ng'ambo




## Majukumu

### Tii sheria za Australia

Wawakilishi wetu katika serikali hutengeneza sheria ili kukuza jamii yenye mpangilio, huru na salama na kulinda haki zetu. Raia wote wa Australia na watu wengine huko Australia lazima watii sheria za Australia.

Maelezo zaidi kuhusu baadhi ya sheria muhimu hapa Australia zinaweza kupatikana katika *Sehemu ya 3, Serikali na sheria hapa Australia.*

### Kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho na mkoa au wilaya, na katika kura ya maoni

Upigaji kura ni jukumu muhimu, haki na upendeleo kwa raia wote wa Australia wa miaka 18 au zaidi.

Ni jukumu la raia wa Australia wa miaka miaka 18 au zaidi kupiga kura katika uchaguzi wa shirikisho na serikali au wilaya, na katika kura ya maoni, ambayo ni kura ya kubadilisha Katiba ya Australia. Kwa kufanya hivi, Raia wa Australia wana msemo katika jinsi Australia inavyotawaliwa na kuchangia katika mustakabali wake.

Upigaji kura ni lazima katika uchaguzi wa shirikisho la Australia na mkoa au wilaya. Inaweza isiwe lazima kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa katika majimbo kadhaa.

Maelezo zaidi kuhusu Katiba ya Australia zinaweza kupatikana katika *Sehemu ya 3, Serikali na sheria hapa Australia*.

### Linda Australia ikiwa kutatokea hitaji

Wahuduma katika jeshi la Ulinzi la Australia ni la kujitolea, jukumu la raia wa Australia ni ku linda Australia lazima kama haja ikitokea. Ni muhimu kwamba raia wote wa Australia wajitolea kuungana pamoja ili kulinda taifa na njia yake ya maisha ikiwa ni lazima.

### Tumikia baraza la wazee kortini ukiitwa kufanya hivyo

Huduma ya baraza la wazee, kama ikitakiwa, ni wajibu kwa raia wa Australia wenye umri wa miaka 18 au zaidi. Baraza la wazee ni kundi la wanaume na wanawake wa kawaida wa Australia ambao husikiza ushahidi kortini na kuamua ikiwa mtu ana hatia au la.

Raia wa Australia ambao wako kwenye jukumu la uchaguzi wanaweza kuitwa kutumikia katika baraza la wazee. Huduma ya baraza la wazee husaidia kuhakikisha kwamba mfumo wa korti unakuwa wazi na kutenda haki.

## Fursa

### Omba kazi katika Huduma ya Umma ya Australia na Jeshi la Ulinzi la Australia

Upendeleo wa raia wa Australia ni kuweza kuomba kazi katika Huduma ya Umma na kufanya kazi kwa Serikali ya Australia kwa mfano, katika Services Australia au Ofisi ya Ushuru ya Australia (ATO).

Raia wa Australia wana haki ya kuomba kazi katika Jeshi la Ulinzi la Australia (Jeshi, Jeshi la Wanamaji, na Wanahewa).

### Kuwania uchaguzi wa bunge

Raia wa Australia wa miaka 18 au zaidi, na ambao hawana uraia wa pili wanaweza kuwania uchaguzi bungeni katika kiwango cha shirikisho,mkoa au wilaya. Ni heshima na jukumu kubwa kuhudumu katika bunge la Australia.

### Kuomba pasi ya Australia na kuingia tena Australia huru

Wakati umekuwa raia wa Australia, una haki ya kuishi huru Australia. Una upendeleo wa kuomba pasipoti ya Australia. Kama ukisafiri nje ya nchi ukiwa kama raia wa Australia, uko huru kusafiri ng'ambo na kurudi Australia.

### Kupokea msaada kutoka kwa afisa wa Australia ukiwa ng'ambo

Katika nchi nyingi, Australia ina ubalozi, balozi kuu au kibalozi. Wakati ukiwa ng'ambo, unaweza kuomba msaada kutoka kwa afisa wa seriklai ya Australia wakati wa hitaji. Hii ni pamoja na wakati wa dharura kama mzozo wa kindani na maafa asilia.

Maafisa wa Australia wanaweza pia kusaidia raia wa Australia nje ya nchi kwa pasipoti za dharura, na kutoa ushauri na msaada katika hali ya ajali, ugonjwa mkali au kifo.

Wakati uko katika nchi nyingine, lazima utii sheria za nchi hiyo.

### Omba watoto waliozaliwa ng'ambo ili wawe raia wa Australia kwa ukoo

Raia wa Australia wanaweza kuombea watoto walizaliwa nje ya nchi ili kuwa raia wa Australia kwa ukoo.

# Kushiriki katika jamii ya Australia

Australia inahimiza raia wake wote kushiriki kwa bidii katika jamii. Raia hai wanachukua jukumu na fursa ya kutengeneza mustakabali wa Australia Kwa mfano, unaweza kujiunga na jumuia na mashirika ya jamii ya ndani, kujitolea kufanya kazi ya kijamii na jamii, kujiunga na sanaa au shirika la kitamaduni, na kushiriki kikamilifu katika maisha ya kisiasa.

Kulipa ushuru ni njia nyingine muhimu ya kuchangia moja kwa moja jamii ya Australia na inatakiwa kisheria. Ushuru hulipwa kutoka kwa pesa unazopata, ikiwa ni kutoka kazini, biashara au vitega uchumi, na inakusanywa na ATO. Kuna ushuru pia kwenye bidhaa na huduma nyingi. ATO hufanya kazi kuhakikisha raia wote wanajua haki zao za ushuru na majukumu yao kulipa kiwango sawa cha ushuru.

Fadhila nyingi ambazo Australia hufurahia leo huweseshwa kupitia ushuru. Ushuru hutumika kwa huduma ambazo ni pamoja na afya, elimu, ulinzi, barabara na reli, na pesa ya kusaidia wasiojiweza.

Kwa kufanya kazi na kulipa ushuru, unaweza kusaidia serikali kutoa huduma hizi muhimu kwa jamii ya Australia. Serikali za jimbo na wilaya na baraza za mtaani pia hukusanya ushuru kupilia huduma. Huduma hizi zinasaidia kufanya Australia kuwa nchi yenye amani na ufanisi leo.



# SEHEMU YA TATU

## Serikali na sheria nchini Australia

# Serikali na sheria nchini Australia

Katika hafla ya uraia, unaapa kufuata na kutii sheria za Australia. Demokrasia ya bunge Mfumo wa serikali ya Australia ni demokrasia ya bungeni. Ni muhimu kwako kuelewa mfumo wa serikali ya Australia, jinsi sheria huundwa katika bunge letu la kidemokrasia na jinsi sheria hizi hutekelezwa. Ni muhimu pia kuelewa jinsi, kama raia, utaweza kusema kuhusu nchi inavyoongozwa.

## Ninawezaje kusema?

### Upigaji kura

Kama ilivyoelezwa katika sehemu ya pili, hapa Australia, raia walio na miaka 18 na zaidi lazima wajiandikishe katika uchaguzi wa shirikisho, mkoa na wilaya na katika kubadilisha katiba.

Katika demokrasia ya bunge la Australia, raia wanasema jinsi Australia itaongozwa na kupiga kura kwa mtu ili kuwawakilisha bungeni. Ikiwa haujajiandikisha sahihi, hauwezi kupiga kura katika uchaguzi.

Upigaji kura ni lazima katika uchaguzi wa Australia, au ikiwa kuna pitisho katika mabadiliko ya katiba.

Tume ya uchaguzi ya Australia (AEC) ni shirika la Jumuiya ya Madola lenye dhamana ya kufanya uchaguzi wa shirikisho na pitisho la mabadiliko, na kudumisha gombo la uchaguzi la Jumuiya ya Madola. AEC haitegemei serikali. Vyama vya kisiasa au watu katika serikali hawawezi kushawishi maamuzi ya AEC.

Katika Australia, kura hupigwa katika sanduku za siri, kwa hivyo uko huru kupiga kura kwa mgombea wowote. Hakuna anayeruhusiwa kujua ambaye umepiga kura, isipokuwa kama utachagua kuwaambia. Usipopiga kura katika uchaguzi na hauna sababu nzuri ya kutopiga kura, unaweza kulazimaka kulipa faini. Upigaji kura kwa lazima ni njia ya kuhakikisha kwamba watu wanaochagua watu ambao wataongoza na kuwakilisha bungeni.

### Kuibua maswala na wawakilishi wako

Raia wa Australia wanaweza kuwasiliana na mwakilishi wao aliyechaguliwa ili kusema wasiwasi zao kuhusu sera ya serikali. Katika njia hii, Waaustralia wote wanaweza kuwa na kitu cha kusema katika kuunda sheria na sera za serikali. Ikiwa raia anawaambia mwakilishi wake aliyechaguliwa kuwa sheria inapaswa kubadilishwa, mwakilishi aliyechaguliwa anapaswa kuzingatia kile ambacho kimependekeza.

# Je! tuliundaje mfumo wetu wa serikali?

## Shirikisho

Baada ya makazi wa Waingereza na Kabla ya 1901, Australia ilikuwa na koloni sita tofauti za Waingereza, zenye uongozi wa binafsi.

Kila koloni ilikuwa na katiba lake na sheria zake kuhusu ulinzi, uhamaji, ada ya barua, biashara na usafiri. Hata hivyo, hii ilileta changamoto kati ya makoloni. Kwa mfano, biashara na usafiri kati ya makoloni ilikuwa ghali na polepole, na kutekeleza sheria katika mipaka ilikuwa ngumu. Koloni tofauti pia zilikuwa na mfumo legevu wa ulinzi.

Matokeo yake, watu walitaka kuunganisha koloni kuunda taifa moja. Muhimu zaidi utambulisho wa kitaifa cha Australia kilikuwa kimeanza kuundwa. Timu za michezo zilikuwa zinawakilisha Australia kimataifa na utamaduni wa kipekee wa Australia ulianza katika nyimbo zinazojulikana, mashairi, hadithi na sanaa.

Kuunganisha taifa ilikuwa ngumu, lakini baada ya muda, wazo la Australia moja liliwezekana. Mnamo 1 Januari 1901, koloni ziliungana kuwa shirikisho la mikoa inayoitwa Jumuiya ya Madola ya Australia.

## Katiba ya Australia

*Sheria ya Katiba ya Jumuiya ya Madola ya Australia 1990 (Katiba ya Australia)* ndio hati halali ambayo inaelezea sheria muhimu za serikali ya Australia. Katiba ya Australia ilipitishwa kama sehemu ya Sheria ya Bunge ya Uingeleza mnamo 1 Januari 1900. Mnamo 1 Januari 1901, Katiba ya Australia ilianza kufanya kazi, koloni za Australia zilikuwa taifa huru, Jumuiya ya Madola ya Australia.

Katiba ya Australia ilianzisha Bunge ya Jumuiya ya Madola ya Australia, iliyoundwa na Jumba ya Wawakilishi na Seneti. Katiba pia iliaanzisha Mahakama Kuu ya Australia, ambayo ina nguvu ya kutekeleza na kufafanua sheria za Australia.

Watu wa Australia wanaweza kubadilisha katiba ya Australia kwa kupiga kura katika kura ya maoni, kama vile kura ya 1967 ya maoni ambapo zaidi ya asilimia 90 ya Waaustralia walipiga kura 'Ndiyo' ili kuruhusu watu wa Aboriginal kuhesabiwa katika sensa.

Katika kura ya maoni, kunahitajika kuwa na idadi kubwa mara mbili ya watu kwa Katiba ya Australia kubadilishwa. Hii inamaanisha, idadi kubwa ya wapigaji kura wa jimbo na idadi kubwa ya wapigaji kura kote nchini laizima wapige kura kwa badiliko hilo. Katiba ya Australia.




Katiba ya Australia

# Je! nguvu ya serikali inathibitiwa vipi?

Katiba ya Australia hugawanya nguvu za serikali kati ya wabunge (bunge), Mtendaji (kwa mfano Waziri mkuu na mawaziri) na mamlaka ya kisheria (majaji), kuacha mtu mmoja, au kikundi kimoja, kutokana na kushikilia nguvu zote za madaraka.

## Nguvu ya kisheria

Nguvu ya bunge ni nguvu ya kuunda sheria. Bunge ina nguvu ya kutengeneza na kubadilisha sheria katika Australia. Bunge ina wawakilishi ambao wamechaguliwa na watu wa Australia.

## Nguvu kuu

Nguvu kuu ni nguvu ya kutekeleza sheria. Watendaji ni pamoja na Waziri Mkuu na mawaziri wa Serikali ya Australia na Gavana Mkuu. Mawaziri wana wajibu wa Idara za serikali.

## Nguvu za hakimu

Majaji wana nguvu kutafsiri na kutekeleza sheria. Korti na majaji ni huru ya bunge na serikali.

Nguvu zimeandikwa katika Katiba ya Australia.

# Je! ni nani ndiye Mkuu wa Nchi ya Australia?

Mkuu wa nchi ya Australia ni Mfalme wa Australia, Mtukufu Mfalme Charles III.


Mfalme wa Australia huteua Gavana Mkuu kama mwakilishi wake katika Australia, kwa ushauri kutoka kwa Waziri Mkuu wa Australia. Gavana Mkuu hutenda bila kutegemea vyama vyote vya kisiasa. Mfalme hana jukumu la kila siku katika kuongoza serikali.

Katika kila jimbo kuna gavana anayewakilisha Mfalme katika jukumu ambalo linalolingana na Gavana Mkuu.

## Utawala wa Kikatiba

Australia ni ufalme kikatiba, ambayo ina maana kwamba Mfalme ni Mkuu wa Nchi ya Australia, lakini anafanya kazi kwa mujibu wa katiba. Kwa kuwa Mfalme haishi nchini Australia, madaraka yake yanapewa Gavana Mkuu wa Australia.

Mfumo wa Australia wa demokrasia ya bunge unaonyesha mila za Uingereza na Amerika ya Kaskazini pamoja kwa njia ambayo Australia inakuwa ya kipekee. Ufalme wa kikatiba ni nchi ambapo mfalme au malkia ndiye mkuu wa nchi lakini lazima atende kulingana na katiba.



Mtukufu Mfalme Charles III

## Jukumu la Gavana Mkuu

Gavana mkuu sio sehemu ya serikali na lazima asitegemee upande wowote.

Kazi ya Gavana Mkuu inajumuisha:

- kusaini hati zote zinazopitishwa na Bunge la Australia kuwa sheria (hii inaitwa Idhini ya Kifalme)
- kuongoza kazi za hafla
- kuidhinisha uteuzi wa Serikali ya Australia na mawaziri wake, majaji wa shirikisho na maafisa wengine
- kuanza mchakato wa uchaguzi wa shirikisho
- kukaimu kama kamanda mkuu wa jeshi la Ulinzi la Australia.

Gavana Mkuu pia ana nguvu maalum zinazojulikana kama 'nguvu zilizotengwa' ambazo zinaweza tu kutumika katika hali mahususi.

# Je! ni nani baadhi ya viongozi wa Australia?

### Mkuu wa Nchi
Mfalme wa Australia

### Gavana Mkuu
Mwakilishi wa Mkuu wa Nchi ya Australia

### Gavana
Mwakilishi wa Mkuu wa Nchi ya Australia katika kila mkoa

### Waziri Mkuu
Kiongozi wa Serikali ya Australia

### Mbunge Mkuu
Kiongozi wa serikali ya jimbo

### Waziri Mkubwa
Kiongozi wa serikali ya wilaya

### Waziri wa Serikali
Mbunge aliyeteuliwa na kiongozi wa serikali kuwajibikia eneo la serikali

### Mbunge (MP)
Mwakilishi aliyeteuliwa na watu wa Australia katika bunge la Australia na bunge la jimbo

### Seneta
Mwakilishi aliyeteuliwa wa jimbo au wilaya katika Bunge la Australia

### Meya au Rais wa Mkoa
Kiongozi wa baraza la serikali ya mtaa

### Diwani
Mwanachama aliyeteuliwa na baraza la mtaani

# Australia inaongozwa vipi?

## Serikali ya Australia

Serikali ya Australia pia inaitwa Serikali ya Shirikisho au Serikali ya Jumuiya ya Madola.
Serikali imeundwa na wabunge wa Bunge la Australia lenye Nyumba mbili:

- wawakilishi wa Jumba
- Seneti.

Katika uchaguzi wa shirikisho, raia wa Australia hupiga kura katika kuchagua wawakilishi wa kila Jumba Uraia.

## Wawakilishi wa Jumba

Nyumba ya wawakilishi ni moja ya nyumba katika Bunge la Australia. Majina mengine ya Wawakilishi wa Jumba hujulikana kama Jumba la Chini au Jumba la Watu.

Australia imegawanywa katika makundi ya shirikisho ya wapigakura. Wabunge (MPs) wanawakilisha watu katika wapiga kura wao.

Idadi ya Wabunge kwa kila jimbo na wilaya huwa kwenye msingi wa saizi ya idadi ya watu katuka mkoa au wilaya. Kwa ujumla, kuna wanachama zaidi ya 150 wanaochaguliwa kwenye nyumba ya wawakilishi.

Wabunge wa bunge na maseneta wanajadili sheria mpya katika Bunge la Australia. Kazi muhimu ya Jumba la Wawakilishi ni kuzingatia, kujadili na kupiga kura mapendekezo ya sheria mpya au mabadiliko ya sheria, na kujadili masuala ya umuhimu wa kitaifa.



Wawakilishi wa Jumba

## Seneti

Seneti ni nyumba nyingine katika Bunge la Australia. Seneti nyakati zingine huitwa Jumba la Juu, Jumba la Kuhakiki au Jumba la Majimbo. Wapiga kura kutoka kila nchi wanawachagua maseneta kuwawakilisha katika Seneti. Majimbo yote huwakilishwa katika Seneti, bila kujali ukubwa na idadi ya watu. Kuna jumla ya maseneta 76. Kila mkoa unachagua maseneta 12, na wilaya ya mji mkuu wa Australia na eneo la Kaskazini huchagua maseneta wawili kila mmoja.

Maseneta pia huzingatia, hujadili na kupigia kura sheria mpya au mabadiliko ya sheria, na kujadili masuala ya umuhimu wa kitaifa.



Seneti

## Serikali ya jimbo na wilaya

Kuna majimbo sita na wilaya mbili za nchi kuu hapa Australia. Kila mkoa una bunge na katiba yake. Serikali za jimbo na wilaya ziko kwa msingi wa miji yao mikuu. Kiongozi wa serikali ya jimbo ni Mbunge mkuu na kiongozi wa serikali ya wilaya ni Waziri Mkubwa.

Serikali za Jimbo huendeshwa kwa njia sawa na Serikali ya Australia. Katika kila jimbo, Gavana huwakilisha Mfalme wa Australia. Katika Wilaya ya Kaskazini, Msimamizi huteuliwa na Gavana Mkuu. Wajibu na majukumu ya Msimamizi ni sawa na zile za Gavana wa jimbo.

Mikoa ina haki ya kutambuliwa na katiba wakati wilaya hazina hiyo. Mikoa ina uwezo wa kupitisha sheria katika haki zao wenyewe wakati sheria za wilaya za kujitawala zinaweza kubadilishwa au kukataliwa na serikali ya Australia wakati wowote.

Katika uchaguzi wa mkoa na wilaya, raia wa Australia wanapiga kura kumchagua mwakilishi wa eneo lao. Wawakilishi huwa mwanachama wa bunge ya mkoa au wilaya.

## Serikali za mitaa

Majimbo na Wilaya za Kaskazini zimegawanywa katika maeneo ya serikali ya mitaa, ambayo inaweza kuitwa jiji, vijiji, miji au manispaa. Kila eneo lina baraza lake la mtaa. Baraza zinawajibika kwa kupanga na kuwasilisha huduma kwa jamii yake ya eneo. Raia katika kila eneo la serikali za mitaa hupiga kura kuteua madiwani wao wa mitaa.

# Je! viwango vitatu vya serikali hufanya nini?

Tofauti kuu kati ya viwango vitatu vya serikali ni kwamba, ingawa baadhi ya majukumu yanaweza kupishana, kwa kawaida kila ngazi ya serikali hutoa huduma tofauti.

### Serikali ya Australia inawajibika kwa:

ushuru

usimamizi wa uchumi wa kitaifa

uhamaji na uraia

msaada wa ajira

huduma za posta na mtandao wa mawasiliano

ruzuku ya serikali (pensheni na msaada wa familia)

ulinzi

biashara na mauzo

uwanja wa ndege na usalama wa angani

maswala ya nje (mahusiano na nchi zingine).

### Serikali za jimbo na wilaya zinawajibika haswa kwa:

hospitali na huduma za afya

shule

barabara na reli

misitu

huduma za polisi na ambulansi

usafiri wa umma.

### Serikali za (na Serikali ya Mpaka Mkuu wa Australia) mitaa zinawajibika kwa:

ishara za mitaa, vithibiti trafiki

barabara za mitaa, njia, daraja

mifereji

mbuga, viwanja vya michezo, madimbwi ya kuogelea, viwanja

viwanja vya kupiga kambi na misafara

uchunguzi wa chakula na nyama

uhibiti wa kelele na wanyama

ukusanyaji taka

maktaba, ukumbi na vituo vya jamii wa mitaa

maswala fulani ya utunzaji wa watoto na wazee

hati za kujenga

mipango ya jamii

maswala ya mazingira ya mitaa.

# Je! vyama vya kisiasa vina jukumu gani katika njia Australia inavyoongozwa?

Chama cha kisiasa ni kundi la watu wanaoshiriki maoni sawa juu ya vile nchi inapaswa kuongozwa. Wao hufanya kazi pamoja kubadili maoni ya chama kuwa sheria. Vyama vikuu vya kisiasa hapa Australia ni Chama cha Wafanyikazi cha Australia (Australian Labor Party), Chama cha Uhuru cha Australia (Liberal Party of Australia), Wakitaifa (Nationals) na Kijani kibichi cha Australia (Australian Greens).

Wabunge wengi wako katika vyama vya kisiasa. Baadhi ya wabunge hawako katika chama chochote cha kisiasa, na wanaitwa 'wakujitegemea '.

Hapa Australia, uko huru kujiunga na chama chochote cha kisiasa ukichagua.

# Je! Serikali ya Australia inaundwa vipi?

Baada ya uchaguzi wa shirikisho, serikali ya Australia huundwa na chama cha kisiasa au muungano wa vyama ulio na wanachama wengi kwenye Jumba la Wawakilishi. Kiongozi wa chama hiki huwa kiongozi wa Serikali ya Australia: Waziri Mkuu.

Baada ya uchaguzi wa shirikisho, chama au muungano wa vyama ulio na idadi ya pili kubwa ya wanachama kwenye Jumba la Wawakilishi huunda Upinzani. Kiongozi wake anajulikana kama Kiongozi wa Upinzani.

Waziri Mkuu anapendekeza wanachama wa Baraza la wawakilishi au maseneta kuwa mawaziri katika serikali ya Australia. Gavana-Mkuu huthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu na mawaziri.

Mawaziri wa Serikali huwajibika kwa maeneo muhimu ya serikali (inajulijkana kama orodha ya kazi) kama ajira, maswala ya Watu wa asili, au Hazina. Mawaziri walio na Uwaziri mkubwa zaidi huunda Baraza la mawaziri, ambalo ndio wa mhimu katika kufanya maamuzi wa Serikali ya Australia.

# Je! sheria huundwa vipi?

Bunge la Australia lina uwezo wa kuunda na kuafanya mabadiliko ya sheria kufaidisha taifa.

Kama mbunge wa Bunge la Australia hupendekeza sheria mpya au mabadiliko kwa sheria, hayo mapendekezo yanaitwa mswada.

↓

Jumba la Wawakilishi na Seneti huzingatia, hujadili na hupiga kura ikiwa wanakubali Mswada.

↓

Ikiwa idadi kubwa ya watu katika Jumba la Bunge wanakubali Mswada, huwa inaenda kwa Gavana Mkuu.

↓

Kwa ujumla, Gavana anaweka muswada ili iwe sheria. Hii inaitwa Idhini ya Kifalme.

Bunge za Jimbo na wilaya huunda sheria zao kwa njia sawa.




# Je! sheria hutekelezwa vipi?

## Korti

Mahakama za Australia zinajitegemea. Korti huamua ikiwa mtu amevunja sheria au kutovunja sheria na huamua adhabu. Korti zinaweza kuweka maamuzi yao kwa msingi wa ushahidi ulio mbele yao.

## Majaji na mahakimu

Jaji au hakimu mkuu ndiye mamlaka ya juu kortini. Wanajitegemea na hakuna mtu anaweza kuwaambia cha kuamua.

Majaji na mahakimu huteuliwa na serikali, lakini serikali haiwezi kuchukua kazi zao ikiwa haikubaliani na maamuzi yao.

## Baraza la wazee la Mahakama

Katika mfumo wa Mahakama ya Australia, watu wanachukuliwa kuwa hawana hatia mpaka wapatikana na hatia mahakamani. Kila mtu ana haki ya kuwakilishwa na wakili kortini.

Korti itatumia baraza la wazee katika hali zingine kuamua ikiwa mtu amevunja sheria. Jukumu la majaji ni kuamua mahakamani ikiwa mtu hana hatia au mwenye hatia. Baraza la wazee ni kundi la watu wa kawaida ambao huchaguliwa bila uratibu kutoka kwa idadi ya watu. Jaji hufafanua sheria kwa baraza la wazee. Katika usikilizaji wa uhalifu, baraza la wazee wakipata mtu ana hatia, jaji huamua adhabu.

## Polisi

Polisi hukuza amani na mpangilio katika jamii. Ni kazi yao kulinda maisha na mali. Hawategemei serikali. Ikiwa polisi wanaamini kwamba mtu amevunja sheria, wanaweza kuwashika na kuwaleta mbele ya korti ya sheria. Polisi wanaweza kutoa ushahidi kortini, lakini korti huamua ikiwa mtu ana hatia au la.

Majimbo na Wilaya za Kasazini zina jeshi lao la polisi. Wao hushugulika na uhalifu chini ya sheria za jimbo na wilaya.

Australia pia ina polisi la kitaifa linaloitwa Polisi wa Shirikisho wa Australia (AFP). AFP huchunguza uhalifu dhidi ya sheria la shirikisho, kwa mfano, ulanguzi wa madawa ya kulevya, uhalifi dhidi ya usalama wa taifa na uhalifu dhidi ya mazingira. AFP pia wanawajibikia kazi ya jumla ya polisi katika Wilaya Kuu ya Australia.

Polisi na jamii wana uhusiano mwema nchini Australia. Unaweza kuripoti uhalifu na kutafuta msaada kutoka kwa polisi wa eneo lako.

Katika Australia, ni kosa la jinai kuhonga afisa wa polisi. Ni kosa la jinai hata kutaka kutoa hongo kwa afisa wa polisi.

## Hatia za uhalifu hapa Australia

Ni muhimu kwako kujua sheria za Australia, kwa sababu kutojua sheria sio sababu ya kuzivunja. Kama wewe ukivunja sheria ya Australia ambayo haukuijua, unaweza kushtakiwa, maana kutokuijua sheria si kisingizio.

Baadhi ya hatia mbaya zaidi ni pamoja na kuua, kuvamia, kuvamia cha kingono, uhasama dhidi ya watu au mali, wizi wa mabavu au wizi, kuwa na uhusiano wa kingono na watoto au vijana ambao wako chini ya umri halali, uendeshaji hatari wa gari, umiliki na utumizi wa madawa ya kulevya na utapeli.

Kila mmoja na haki ya kujisikia vizuri na familia zao, marafiki na wale wanaowapenda. Kama vile katika nchi zingine, uhasama kwa mtu mwingine ni kinyume cha sheria nchini Australia na ni uhalifu mbaya sana. Hii ni pamoja na uhasama nyumbani na katika ndoa, inayojulikana kama uhasama au vurugu za familia. Vurugu za ndani na za familia ni pamoja na tabia au vitisho ambavyo vina lengo la kudhibiti mpenzi kwa kusababisha hofu au kutishia usalama wao. Vurugu za ndani na za familia hazikubaliki na ni kinyume cha sheria. Vurugu za familia na mjumbani zinaweza kujumuisha kupiga, kutenga ndugu wa familia na marafiki na familia, au kutishia watoto au wanyama wa kufugwa.

Mtu anayetenda uhalifu huu anaweza kwenda jela, iwe ni mwanaume au mwanamke. Hakuna mtu ambaye anatakiwa kukubali kuchukuliwa vibaya au kuumizwa.

Kama wewe au mtu mwingine unayemjua yuko hatarini unatakiwa kuwasiliana na polisi. Habri zaidi zinapatikana kwenye www.respect.gov.au na www.1800respect.org.au

## Hatia za Trafiki

Sheria za trafiki na barabara huthibitiwa na serikali za jimbo na wilaya. Watu wanaweza kutozwa faini kubwa au hata kutumwa jela kwa kuvunja sheria za trafiki. Kuendesha gari Australia, lazima uwe na leseni ya kawaida ya kuendesha gari na lazima gari limesajiliwa.

Kila mtu anayesafiri kwa gari lazima avae mkanda. Watoto wachanga lazima wawekwe katika kiti cha gari kilichoidhinishwa. Sheria za barabarani ni kali sana. Ni haramu kuendesha gari baada ya kutumia madawa ya kulevya au kama wewe uko juu ya kikomo cha pombe kwenye damu. Ni kinyume na sheria pia kutumia simu ya mkononi unapoendesha gari.



# SEHEMU YA 4

# Maadili ya Australia



# Maadili ya Australia

Maadili ya Australia yamejegwa kwenye uhuru, heshima, bila upendeleo na usawa ni muhimu kwa jamii yetu kubakia salama, yenye mafanikio na ya amani.

Maadali yetu yameunda nchi yetu na utamaduni wetu na ndio sababu watu wengi wanataka kuwa raia wa Waaustralia.

Uraia wa Australia ni juu ya kuishi kwa kufuata thamani hizi katika maisha yako ya kila siku na jamii ya mahali. Kwa hivyo ni muhimu kwamba uelewe maadili haya ambayo watu wote wa Australia wanatarajiwa kuziheshimu na kuzifuata.

## Maadili yetu

### Uaminisho wa Utawala wa sheria

Waaustralia wote wanalindwa na sheria zetu na muundo wa kisheria. Waaustralia wanatambua thamani ya sheria katika kukuza amani na jamii yenye mpangilio.

Chini ya utawala wa sheria, Waaustralia wote ni sawa chini ya sheria na hakuna mtu au kundi liko juu ya sheria. Nchini Australia, kila mtu anapaswa kutii sheria wakati wowote na sio kuzivunja, vinginevyo unaweza kulipishwa faini. Unapaswa kufuata sheria hata kama hakuna mtu wa ku kuangalia.

Sheria za Australia zinatumika kwa watu wote wa Australia. Hii inamaanisha bila kujali asili au utamaduni yako, lazima ufuate sheria za Australia.

### Demokrasia ya bunge

Demokrasia ya bunge Mfumo wa serikali ya Australia ni demokrasia ya bungeni. Sheria zetu zinaamuliwa na wabunge waliochaguliwa na watu. Hii inaaanisha kwamba raia wate wa Waaustralia wanahusika katika jinsi nchi inaongozwa. Nguvu ya serikali inatoka kwa watu wa Australia kwa sababu raia wa Australia hupiga kura kwa watu kuwawakilisha bungeni.

Upigaji kura ni lazima nchini Australia. Hii inaonyesha umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi.

## Uhuru wa kusema

Watu wa Australia wanapaswa kuwa na uwezo wa kueleza mawazo yao kwa uhuru watakavyo, cha mhimu iwe ndani ya sheria. Katika Australia, watu wako huru kukutana katika mahali pa umma au pa siri kwa mjadala wa kijamii au kisiasa. Watu wako huru wa kuzungumza na kuandika wanachofikiria na kujadili mawazo yao na wengine. Magazeti, runinga na redio zina uhuru sawa.

Waaustralia wanaruhusiwa kupinga vitendo vya serikali, kwa sababu uvumilivu wa maandamano ya umma ya amani ni sehemu muhimu ya demokrasia.

Kamwe haikubaliki kukuza vurugu dhidi ya mtu mwingine au kikundi cha watu (kama vile kwa sababu ya utamaduni wao, ukabila, dini au usuli) kwa sababu ni kinyume na maadili ya Australia na sheria. Pia ni kinyume cha sheria kufanya madai ya uongo au kuwahimiza wengine kuvunja sheria. Uhuru wa watu wengine wa kujieleza na uhuru wa kujieleza unapaswa kuheshimiwa, kitu cha mhimu msemo huo uwe halali.

## Uhuru wa ushirika

Katika Australia, watu wana uhuru wa kujiunga au kuondoka kwenye kikundi chochote kwa hiari kama ilivyo ndani ya sheria. Waaustralia wana uhuru wa kuungana na shirika la kisheria, kama vile chama cha kisiasa, chama cha biahara, dini, kundi la kitamaduni au kijamii. Watu binafsi hawawezi kulazimishwa kujiunga shirika au kulazimishwa kulitoka.

Waaustralia wanaweza kuja pamoja kwa uhuru, ikiwa ni pamoja na kupinga hatua ya serikali au shirika. However, all protests must be within the law. Walakini, malalamishi yote lazima yawe ndani ya sheria. Hii inamaanisha lazima ziwe za amani, na lazima zisiumize mtu yeyote au kuharibu mali.

## Uhuru wa dini

Australia haina dini la taifa na Watu hapa Australia wako huru kufuata dini yoyote wanayochagua. Serikali inatendea raia kwa usawa, haijalishi dini au imani yao. Hata hivyo, vitendo vya kidini lazima visivunje sheria za Australia.

Sheria za kidini hazina hadhi ya kisheria nchini Australia. Sheria ya Australia lazima ifuatiwe na kila mtu nchini Australia, ikiwa ni pamoja na pale ambapo ni tofauti na sheria za kidini. Baadhi ya desturi za kidini au kitamaduni, kama vile mitala (kuolewa na zaidi ya mtu mmoja wakati huo huo) na ndoa za kulazimishwa, ni kinyume na sheria nchini Australia na inaweza kusababisha adhabu kali za kisheria, zikiwemo kufungwa jela.

Ukoseaji wa dini haukubaliki katika jamii ya Australia. Watu wote wanapaswa kupewa fursa sawa ya kufuata malengo na maslahi yao bila kujali ukabila au dini yao cha mhimu wawe wanafuata sheria ya Australia.



## Usawa wa watu wote chini ya sheria.

Jamii ya Australia ina thamani ya usawa wa watu wote, bila kujali jinsia zao, mwelekeo wa kijinsia, umri, ulemavu, dini, mbio, au asili ya kitaifa au kikabila. Kuna baadhi ya sheria hapa Austrakia ambazo hukakikisha mtu hatendewi tofauti na wengine.

Sheria inatumika nchini Australia ili watu kutoka asili mbalimbali wasipate upendeleo maalumu, au kuweza kubaguliwa. Kwa mfano, Wabudha na watu wengine wa imani mbalimbali hupokea matibabu sawa kama Wakristo. Chini ya sheria zetu,  watu wawili wanaweza kuoana, ikiwa ni pamoja na ndoa kati ya wanaume wawili au wanawake wawili.

Wanaume na wanawake wana haki sawa nchini Australia na wanapaswa kupewa fursa sawa ya kufuata malengo na maslahi yao. Wanaumena wanawake wana haki sawa kujiunga na elimu na ajiri, wanaweza kucgua, kusimama kwa ajiri ya bunge, wanaweza jiunga na Jeshi la Ulinzi la Australia na polisi, na ni kuchukuliwa sawa katika Mahakama ya sheri.

Ni kinyume cha sheria kubagua mtu kwa sababu ya jinsia yake. Katika Australia, ni haki kwa mwanamke kupata kazi mbele ya mme, kama ana sifa bora na ujuzi.

Wanaume na wanawake wana haki ya kufanya uchaguzi wao binafsi kuhusu maswala kama ndoa na dini, na wanalindwa na sheria ya dhuluma au uhasama. Ukatili wa mwili dhidi ya mwenzi au mpenzi haukubaliki kamwe na ni kosa la jinai katika Australia.

Talaka inakubalika nchini Australia. Ama mume au mke anaweza kuomba talaka mahakamani hata kama mwenzi mwingine anataka kuendelea na ndoa.

## Usawa wa fursa na a ' usawa wa haki '

Tunaamini kwamba kila mtu anastahili ' usawa wa haki ' na haipaswi kunyimwa kwa aina yoyote ya daraja la tofauti. Kila mtu, bila kujali malezi yao, anapewa nafasi sawa ya kufanikiwa katika maisha, kuhakikisha kwamba kila mmoja ana haki sawa ya kisheria kama kitu mhimu katika jamii ya Australia.

Kitu ambacho mtu anafikia maishani mwake kinapaswa kuwa matokeo ya bidii yao na vipawa vyao.  'usawa wa haki' ina maana kwamba mtu anapaswa kupata kazi au cheo kwa msingi wa ustadi wake, uwezo na uzoefu, sio kwa sababu ya asili yake.

Wakati shirika linahitaji kujaza kazi, sheria inaunga mkono kwamba wanachagua mtu aliye na ujuzi bora na uzoefu wa kazi.

Wahamiaji wengi nchini Australia wamekuwa viongozi katika biashara, wataalamu, sanaa, huduma ya umma na michezo kupitia bidii yao na vipawa vyao.



## Kuheshimiana na uvumilivu kwa wengine

Katika Australia, watu binafsi lazima Waheshimu uhuru na heshima ya wengine, na maoni yao na uchaguzi.

Ni kinyume cha sheria kufanya ubaguzi kwa mtu mwingine. Vurugu za aina yoyote, ikiwa ni pamoja na zile za maneno na kimwili, ni kinyume na sheria. Australia inaimani katika mabishano ya amani na zaidi ya yote haki ya kuwa salama na huru kutokana na vurugu pamoja na kutishiwa.

Katika Australia, kuna sheria kali sana kuhusu umri wa ridhaa ya ngono, ambayo ni 16 au 17 kutegemeana na hali au eneo ambalo wewe huishi. Kwa mfano, nchini Australia, mtu wa miaka 20 hawezi kuwa na uhusiano wa kingono na msichana wa miaka 15, kwa sababu hiyo ni kinyume na sheria katika majimbo yote ya Australia na maeneo yote.

Nchini Australia, vitendo halali vya polisi vinapaswa kuungwa mkono. Unapaswa kutii ombi halali kutoka kwa polisi, kwa sababu Waaustralia hutenda kwa kufuata sheria.

Australia ina thamani ya misingi ya kuheshimiana na uvumilivu. Hii ina maanisha kuwasikiliza wengine na kuheshimu maoni na maoni yao, hata wakati wakati wakiwa na mawazo tofauti na yako mwenyewe. Watu wanapaswa kuvumiliana wanapogundua kuwa hawakubaliani.

Ubaguzi hauna nafasi katika Australia. Hii inajumuisha kutengeneza au kuchangia nyenzo mbaya za kimatusi kwenye intaneti au machapisho mengine na kufanya maoni ya kibaguzi katika sehemu za jamii au kwenye tukio la kimichezo.

# Jamii yetu

## Kutoa mchango

Uraia hukupa fursa ya kuhusika kikamilifu katika kujenga maisha ya taifa na jamii. Inamaanisha kwamba uko tayari kutimiza wajibu wako kama raia wa Australia. Waaustralia wanatarajia kila mtu anayeishi Australia kushiriki katika jamii yetu na kuchangia katika jamii yetu. Kila mtu ana jukumu la kujisaidia mwenyewe na familia zao wakati wanaweza kufanya hivyo.

## Huruma kwa wale wanaohitaji

Waaustralia wanathamini ‘kujaliana’. Tunasaidiana na wengine nyakati za mahitaji. Kwa mfano, inaweza kumaanisha kuchukua chakula kwa jirani mzee, kuendeshe rafiki kwenda kwa miadi ya matibabu au kutembelea mtu anayeumwa, asiyejiweza au mpweke.

Katika roho hii ya kujaliana, Australia ina utamaduni dhabiti wa huduma ya jamii na kujitolea- kutazamana na kuimarisha jamii. Kujitolea ni fursa kubwa pia kushiriki maarifa, kujifunza ustadi mpya, na kuongeza hali yako ya kuwa wa jamii ya Australia. Kuna fursa nyingi kwako kujitolea katika Australia.

## Kiingereza kama lugha ya taifa

Jamii ya Australia inathamini lugha ya Kiingereza kama lugha ya kitaifa ya Australia, na kama kiungo muhimu cha jamii. Watu wanaoishi Australia wanapaswa kufanya bidii ya kujifunza Kiingereza.

Ni muhimu kujifunza kuongea Kiingereza kwa sababu inasaidia kupata elimu, kazi, na kujiunganisha vizuri kwenye jamii. Ni muhimu ili ushiriki kiuchumi na mshikamano wa kijamii. Maombi kwa ajili ya uraia wa Australia lazima yafanyike ili kufanya juhusu ya kujifunza lugha ya Kiingereza, kama siyo lugha ya kuzaliwa.

## Kusaidia kufanya jamii yetu kuwa salama

Huko Australia, kila mmoja ana jukumu la kusaidia kulinda jamii ya Australia. Kwa mfano, ikiwa watu huko Australia wanahisia kuwa rafiki yao au jirani anaweza kupanga kitendo cha kigaidi, anapaswa kuripoti kwa mamlaka ya serikali ya Australia haraka iwezekanavyo. Kwa njia hii, tunaweza kusaidia kulinda usalama wa jamii yetu.

Vivyo hivyo, ikiwa mtu huko Australia anaona au ana ufahamu wa mtoto kubakwa, anapaswa kuripoti polisi kwa uchunguzi.

Unyanyasaji wa kwenye mtandao haukubaliki nchini Australia. Hii mda mwingine huitwa unyanyasaji wa kwenye mtandao. Mifano inajumuisha kuchangia picha za ngono au video bila ruhusa, kutukana mtu kwenye mtandao, au kufanya maoni ya matusi kuhusu mtu mwingine mtandaoni. Aina nyingi ya matusi mtandaoni ni kinyume cha sheria nchini Australia.

## Ukalimu wa Australia

Katika hafla ya uraia, raia wa Australia wanaapa uaminifu wao kwa Australia na watu wake. Raia wa Australia wanaweza pia kushikilia uraia wa nchi nyingine au nchi ikiwa sheria za nchi hizo zinaruhusu. Hii inajulikana kama uraia wa pili, au mwingi, uraia. Walakini, hata kama mtu pia ni raia wa nchi nyingine, raia wa Australia ndani ya Australia lazima kufuata sheria zote za Australia wakati wote. Baadhi ya sheria za Australia lazima zifuatwe na raia wa Australia hata wakiwa nje ya nchi. Kwa mfano, ni kinyume kwa raia wa Australia kujihusisha na shughuli zozote za ngono, hapa na nje ya nchi, kwa mtoto wa miaka chini ya 16.

Jamii ya Australia inatokana na majukumu yetu ya pamoja sio kudhoofisha masilahi na usalama wa Australia. Kwa mfano, kutumia mitandao ya kijamii kushiriki siri rasmi za serikali inaweza kunadhoofisha masilahi ya Australia. Vivyo hivyo, kukuza kutokuaminiana na kuogopa jamii ya kikabila kunaweza kuharibu uhusiano wa jamii ya Australia.

Katika Australia, tunakuja pamoja wakati wa magumu na kusaidiana sisi kwa sisi katika nyakati nzuri na mbaya. Wakati wa moto uliokithiri wa msitu wa Australia wa 2019-20, ambao ulisababisha upotezaji mbaya wa maisha, mali na wanyamapori, na uharibifu wa mazingira, jamii nyingi za tamaduni nyingi zilifanya kazi kukusanya pesa, nguo na michango ya chakula kusaidia watu walioathiriwa na moto wa msituni. Kwa mfano, washiriki wa jamii za Wachina, Kivietinamu na Kambodia huko Victoria walikusanya michango katika vituo vya ununuzi na kupata pesa kupitia hafla za vikundi vya jamii, na washiriki wa jamii ya Sikh walichangia maelfu ya chupa za maji kwa jamii na wazima moto huko Queensland.



# Kwa kutamatisha

Taasisi zetu za kidemokrasia na maadili ya Australia tunayochangia yameunda jamii yenye amani na thabiti.

Tuna utamaduni mzuri na wa kipekee kushiriki. Kama raia wa Australia, utakuwa sehemu ya hadithi yetu ya kitaifa na utachangia siku za usoni. Australia inakukaribisha. Uraia ni mapatano yetu ya pamoja.

# Faharasa ya maswali yanayoweza kujaribiwa

alama ya maua
maua ya kitaifa
*Ishara ya maua ya Australia ni ufito wa dhahabu.*

Tume ya Haki za Binadamu ya Australia
Tume huru ambayo inachunguza malalamiko juu ya ubaguzi na ukiukaji wa haki za binadamu.
*Tume huru ambayo inachunguza malalamiko juu ya ubaguzi na ukiukaji wa haki za binadamu.*

bila mapendeleo
kila mtu, bila kujali malezi yao, anapewa nafasi sawa ya kufanikiwa katika maisha
*Katika Australia, tunaamini kuwa kila mtu anastahili "kutendewa sawa".*

chama cha kisiasa
ni kundi la watu wanaoshiriki maoni sawa juu ya vile nchi inapaswa kuongozwa na mara nyingi wanatafuta kuweza kuchaguliwa.
*Wanachama wa chama cha kisiasa hukutana mara kwa mara, kwa mfano, kujadili kuboresha usafiri wa umma.*

demokrasia
serikali na watu kupitia wawakilishi walioteuliwa
*Grace alifurahia kuishi katika demokrasia ambapo angeweza kupigia kura mwakilishi wake bungeni.*

demokrasia ya bunge
mfumo wa serikali ulio kwenye msingi wa uchaguzi wa kawaida wa wawakilishi wa bunge na raia
*Katika demokrasia ya bunge, watu hupiga kura kwa wawakilishi wao.*

Eneo la uchaguzi
wilaya zilizoundwa na wapiga kura wanaopiga kura kuchagua wanasiasa katika Baraza la Wawakilishi
*Wateule huitwa wilaya za uchaguzi, mgawanyiko, au viti.*

hakimu mkuu
jaji (kiongozi) wa korti ya kiwango cha chini
*Hakimu mkuu alipata mwizi na hatia na kumtuma kwa jela.*

heshima
onyesha kujali mtu kama mtu, au uamuzi ambao wamefanya
*Emily alifurahi kuwa familia yake waliweza kuheshimu uamuzi wake wa kuwa Budha.*

Huduma ya Umma ya Australia
idara za serikali na watu walioajiriwa nazo
*Paul alipata kazi katika Huduma ya Umma ya Australia kama afisa wa Services Australia.*

ikoni
Picha-inayojulikana sana
*Jumba la Opera ni alama inayojulikana ya Sydney.*

Katiba
sheria kuu ya Australia ambayo serikali lazima itimize
*Katiba inaweka nguvu za kisheria, mtendaji, na mahakama.*

unyanyasaji wa mtandaoni

Tabia ambazo hutumia taknologia kwa kutishia, kubugudhi, kunyayasa au kutesa mtu mwingine kwa lengo la kuwaumiza.
*Aina nyingi za unyanyasaji wa mtandao ni kinyume cha sheria katika Australia na inapaswa kuripotiwa kwa polisi na huduma ya mtandaoni, kama jukwaa la media ya kijamii, ambayo ilitokea.*

kidunia

kidunia kando na dini
*Katika jamii ya kidunia,  hakuna dini rasmi.*

vurugu za ndani na za familia

Tabia au vitisho ambavyo vina lengo la kudhibiti mpenzi kwa kusababisha hofu au kutishia usalama wao.
*Vurugu za ndani na za familia ni kinyume cha sheria na lazima zitolewe taarifa polisi.*

korti

mahali ambapo kesi za kisheria huongozwa na jaji au hakimu
*Wakati watu wanavunja sheria, wanaweza kwenda kortini.*

kuanzia wakati huu na kuendelea

kuanzia sasa na kuendelea
*Katika hafla ya uraia, unaahidi kuwa mwaminifu wa Australia kuanzia sasa na kuendelea.*

kujali

kusaidia na kupokea msaada kutoka kwa wengine, haswa katika nyakati ngumu
*Wakati gari langu liliharibika, madereva wengine walitusaidia kulisukuma katika moyo wa kujaliana.*

kujitosheleza

kuweza kujipatia mahitaji yako mwenyewe, bila msaada wa watu wengine
*Kuwa na kazi ilimaanisha kwamba alikuwa na uwezo wa kununua chakula chake mwenyewe na kulipa kodi yake mwenyewe. Aliweza kujitosheleza.*

Kundi la Kwanza la Meli (First Fleet)

kundi la meli 11 zilizotoka kwenda Uingereza chini ya Captain Arthur Phillip kuanzisha makazi ya wafungwa huko New South Wales
*Kundi la kwanza la Meli lilitua Sydney Cove mnamo 26 Januari 1788.*

kura ya maoni

kura na wapigaji kura wote kwenye mabadiliko yaliyopendekezwa katika Katiba ya Australia
*Katika kura ya maoni 1967, watu walipiga kura kuhesabu watu Aboriginal kwenye sensa.*

lnguvu ya kutunga sheria

nguvu na mamlaka ya kuunda na kubadili sheria, moja ya nguvu tatu chini ya Katiba ya Australia
*Chini ya katiba, bunge lina nguvu ya kutunga sheria.*

maadili

kanuni zinazosaidia mtu kuamua kitu amacho ni sahihi na au kibaya, na jinsi ya kutenda katika hali mbali mbali
*Australia ina seti ya maadili iliyoshirikiwa, ambayo tunaiita maadili ya Australia.*

mkoa

eneo la serikali ya mitaa
*Barabara katika eneo langu ni salama sana.*

mpangilio

kujenga, kukuza, kuanza
*Gavana Philip alianza koloni ya kwanza huko New South Wales.*

mtu wa kujitolea

mtu anayepeana muda wake kwa mtu au shirika bila kutarajia malipo
*Raza ni mtu wa kujitolea anayefunza watu Kiingereza nyumbani kwao.*

muungano
kuungana na vyama viwili au zaidi, kawaida kuunda serikali au upinzani
*Baada ya uchaguzi, hakuna chama kilicho na watu wengi katika Jumba la Wawakilishi, kwa hivyo vyama viwili vya maoni sawa viliungana kuunda muungano.*

mwakilishi
mtu ambaye hutenda au kusema kwa niaba ya wengine
*Mwakilishi wa baraza la eneo langu alipenda maoni yangu na aliwakilisha katika mkutano wa baraza.*

mzozo wa umma
maandamano na vurugu na idadi kubwa ya watu, kawaida kupinga dhidi ya uamuzi au sera ya serikali
*Kulikuwa na mzozo wa umma wakati serikali ilipitisha sheria zisizopendwa.*

ndoa ya kulazimishwa
ndoa ambapo mmoja wa wenzi wawili hawakuwa na chaguo lao wenyewe
*Hakuwa na furaha kamwe juu ya ndoa yake ya kulazimishwa na kila wakati alitaka kuondoka.*

nguvu kuu
nguvu na mamlaka ya kutekeleza sheria, moja ya nguvu tatu chini ya Katiba ya Australia
*Mawaziri wa Serikali ya Australia na Gavana-Mkuu wana nguvu kuu ya kutekeleza sheria zilizoundwa na Bunge la Australia.*

nguvu za kisheria
nguvu na mamlaka ya kufafanua na kutekeleza sheria, moja ya nguvu tatu chini ya Katiba ya Australia
*Mahakama katika Australia zina nguvu ya kisheria.*

orodha ya uchaguzi
orodha ya watu wanaoweza kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni
*Wakati Jan alifika katika kituo cha kupigia kura, afisa alitafuta jina lake kwenye orodha ya uchaguzi.*

ruzuku ya serikali
malipo ya pensheni au fadila za serikali kusaidia watu ambao hawana kazi, walemavu, wazee na wengine wanaohitaji
*Wakati Trang alipoteza kazi yake, alikuwa ameomba ruzuku ya serikali.*

sanduku la siri
mfumo wa kupiga kura ambapo watu hupiga kura kwa siri, ili hakuna mtu anaweza kushawishi au kushinikiza mwingine kupiga kura kwa njia fulani
*Katika sanduku la siri, hakuna mtu anayetazama wakati unapoandika kura yako.*

ubaguzi
Ubaguzi, ubaguzi wa rangi, unyanyasaji au chuki inayoelekezwa kwa mtu kwa sababu ya asili, rangi, asili ya kabila au kabila.
*Ubaguzi wa rangi ni kinyume cha sheria nchini Australia na ni lazima kutolewa taarifa kwa polisi.*

shirikisho
muungano wa koloni katika taifa moja iliyo ndani ya dani ya koloni zilizozuia nguvu fulani
*Mnamo 1901, koloni ziliungana kuwa shirikisho liitwalo Jumuiya ya Madola ya Australia.*

tekeleza sheria
kuhakikisha kwamba watu wanafuata sheria
*Polisi hutekeleza sheria na kuhimiza amani.*

tume
kundi la watu walio na jukumu rasmi
*Tume inayojitegemea huandaa uchaguzi.*

uchaguzi
tukio ambalo raia huchagua watu wa kuwawakilisha katika bunge
*Raia wa Australia wenye umri wa miaka 18 na zaidi lazima wapige kura katika uchaguzi.*

ufalme wa kikatiba
nchi ambapo mfalme au malkia ndiye mkuu wa nchi, ambaye nguvu zake zimezuiliwa na Katiba
*Katiba yetu ilianzisha Jumuiya ya Madola ya Australia kama utawala wa kikatiba, na Mfalme au Malkia wa Uingereza kama Mkuu wa Serikali yetu.*

uhuru
uhuru wa kibinafsi na uhuru
*Katika jamii yetu ya demokrasia, watu wana uhuru wa kuzungumza, uhuru wa kujielezea, uhuru wa dini na uhuru wa ushirika. Tunathamini uhuru huo.*

ujumuishaji
mchakato wa kubadilika kwa wahamiaji ili waweze kushiriki na kuchangia katika jamii yao mpya inayoibuka
*Kwa wakati, wahamiaji wananufaika kutokana na kujumuishwa kwao Australia na jamii ya wenyeji.*

ulanguzi wa madawa ya kulevya
kubeba au kununua madawa ya kulevya kinyume ya sheria
*Jess alipelekwa jela kwa ulanguzi wa madawa ya kulevya.*

usawa
usawa katika hadhi
*Waaustralia wanaamini katika usawa wa watu wote.*

Service Australia
Wakala wa Serikali ya Australia ambayo hutoa malipo anuwai ya kiafya, kijamii na ustawi kupitia Medicare, Centrelink, na Usaidizi wa Mtoto.
*Services Australia hutoa malipo ya msaada kupitia Centrelink na huduma zingine.*

usiklizaji wa uhalifu
usikilizaji wa ukweli unaofanywa na mahakama ili kuamua kama mtu amepatikana na hatia au hana hatia
*Baada ya usikilizaji wa hatia, mwizi wa benki alipelekwa jela.*

Utawala wa sheria
watu wote, ikiwa ni pamoja na raia na serikali, wamefungwa na sheria
*Kila mtu huko Australia, pamoja na Waziri Mkuu, wamefungwa na sheria zote za Australia chini ya Utawala wa Sheria.*

Watu wa Aboriginal na Torres Strait Islander
Watu wa Aboriginal na Torres Strait Islander ndio watu wa asili na wakazi wa ardhi ya Australia
*Aboriginal na Torres Strait Islander huunda wastani wa asilimia tatu ya idadi ya watu wa Australia.*

Australian Taxation Office (ATO)
Wakala wa Serikali ya Australia ambayo inasimamia mifumo ya ushuru na malipo ya wazee ambayo inasaidia na kufadhili huduma kwa Waaustralia
*Kila mwaka Waaustralia wengi huwasilisha kurudi kwa ushuru kwa Ofisi ya Ushuru ya Australia.*

Watu wa asili
Watu wa Aboriginal na/na Torres Strait Islander wa Australia
*Waaustralia wa asili ni Watu wa Kwanza wa nchi hii.*

Wimbo wa taifa
Wimbo wa taifa
*Wimbo wa taifa wa Australia ni 'Eendeleza Australia bila Mapendeleo' (Advance Australia Fair).*



# Mwisho wa sehemu inayoweza kujaribiwa